

UKIMWI: MAAMBUKUZI KUTOKA KWA MAMA HADI KWA MTOTO

“Mkakati na maingilio ya kuzuia maambukizi ya ukimwi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto ni njia muhimu ya kuimarisha taratibu za kiafya, tokomeza athari za Ukimwi, na kuhamasisha jamii kupigana na Ukimwi”-UNICEF

Kunazo njia nyingi za kuangazia tatizo la Ukimwi duniani. Unaweza kuangazia hali ya wanawake kote duniani – bayana kwamba katika Afrika kuna wanawake kumi na wanne kwa kila wanaume kumi walioambukizwa. Unaweza kuangazia kitengo fulani cha umma, kama vile jumuiya za LGBT ulimwenguni kote, au kuenea kwa virusi miongoni mwa wakaazi wazaliwa. Au unaweza kuangazia tatizo la maambukizi kutoka kwa mama hadi kwa mtoto.

Upitishanji kutoka kwa mama hadi kwa mtoto ni chanzo kikuu cha maradhi ya ukimwi. Inaweza kutukia wakati wa ujauzito, kupitia mazalio, lakini kwa mara nyingi zaidi husazambazwa katika

kujifungua, au kupitia kunyonyesha. Kana njia kadhaa za kupunguza uwezekano wa kuambukizwa. huduma ifaayo wakati wa kujifungua, kwa mfano, inaweza kisitisha kupasuka ambako husababisha damu kupashana, kama ilivyo hali ya kujifungua kupitia upasuaji wa hiali badala ya uzazi wa kawaida(kupitia njia ya uzazi).Hii ingehitanji kuimarisha pakubwa uwezo wa kimatibabu, hasa katika Afrika,

Ambako 95% ya wanawake wajawazito walio na virusi vya ukimwi ulimwenguni ndiko wanakoishi. Kupunguza muda wa kunyonyesha, au kutonyonyesha kabisa, imeonyeshwa kupunguza maambukizi kwa kiwango kikubwa, lakini jambo hili linazua maswala mengi. Kwanza, ni jambo la kawaida wanawake wa Afrika kuwanyonyesha watoto wao hata kwa muda wa miaka miwili, mara nyingi kama njia ya kupanga uzazi. Kupunguza muda huu uwe miezi sita kunaweza to kupunguza hatari ya Kuambukizwa kwa kiwango cha theluthi mbili, lakini kubadili tabia hii ingemaaniza kubadili desturi za kimila.

Kunyonyesha ndio njia salama mno ya wanawake wa Afrika kulisha watoto wao, kwani hupitisha chembe muhimu za kuzuia magonjwa na kuwakinga watoto dhidi ya bakteria apazo huwa kwa maziwa ya kununua iliyo tengeneza kwa maji machafu. Mbinu za kampuni zinazounda maziwa ya unga

zajulika vyema. Baadhii ya kampuni zimeingiliwa kwa mabana na shirika la WHO kwa kukosa kuchapisha maelezo katika mabandiko ya mikebe kwa lugha za jamii ndogo au kuweka picha zenye maelezo, kwa wamama wasionjua kusoma.

Bei ya maziwa ya kununa ni ghali mno kiwango kuwa ni kawaida kwa familia kiwalisha watoto maziwa ya unga na kuwafisha njaa pasipo kufahamu. Vifo aya watoto wachanga vinavyo sababishwa na kuhara na kutopata chakula cha kutosha mara nyingi uhusishwa na maziwa ya kununua ambayo ni hafifu sana, au iliyochanganywa na maji machafu.

Wanawake maskini, ambao hapa mwanzoni waliambiwa kwamba kunyonyesha ni mwafaka zaidi kwa watoto wao, hivi sasa wanashauriwa kwamba maziwa yao wenyewe wanyeza kuambuziza wanao na Ukimwi. Ilhali Watoto wachanga wasiponyonyeshwa wamo hatarini mara sita zaidi ya kufariki katika miezi miwili ya kwanza ya maisha yao.

Maambukizi kupitia kunyonyesha yaweza kupunguzwa kwa kuhudumia mapema vindonda au vipele vyovyote katika matiti au modomo wa mtoto, bali kwa upande wa kujifungua, kunahitajika muundo-msingi wa kimatibabu ambau haumo kwa sasa.

Baadhi ya mataifa kama vile Brazil, suluhisho bunifu zimepatikana, kama vile benki za maziwa ya mama, wauguzi na kupasha maziwa moto kabla ya kunywesha watoto. Njia hizi zimepatikana kuwa na mafanikio, walakini, mafunzo mengi na ufadhili zinahitajika kupewa wamama.

Matitbabu ya msingi kwa wanawake wajawazito walio na virusi vya Ukimwi ni dawa za kupunguza makali ya ukimwi, ambayo kwa kawaida hupeanwa kabla na wakati wa kujifungua.

Ingawa madawa haya yameonyeshwa kuwa na manufaa, utata mwingi kuhusu matumizi yake.

Watu wengi barani Afrika hawaamini kuwa madawa yanaweza kusaidia hali ya maradhi ya ukimwi, au hajapata habari kususumu matumizi yake, ama hawana maji masafi ya kuzinywea.

Utumizi wa madawa katika kupunguza idadi ya maambukizi kupitia kwa mama pia umezua masala magumu katika sekta ya mashirika yanayo husika na madawa na jinsi yanavyo saidia katika huduma za afya ya umma

Mojawapo ya madawa yanayopatikana kwa urahisi iitwayo AZT, imesisimsha kashifa na tuhuma kwa kukisiwa kwaha ina madhara baada ya matumizi..

Kisiki kingine katika kipigana na Ukimwi katika Afrika ni bayana kwamba madawa badia yamepenya barani. Mara nyingi madawa haya hutoka katika viwanda vya uchina ambavyo huunda madawa badia yasiyo na uwezo wa kutibu.

Mara kwa mara wanawake wanaotumia madawa haya hufa, hivi kueneza zaidi tuhuma kuhusu umuhimu wa madawa.

Tena, kuna swala la Bei ghali abalo limejitokeza wazi wazi. Mojawapo ya madawa ya kupunguza makali ya ukimwi inayopatikana kwa urahisi iitwayo, Nevirapine, hugharimu dola 8 za Marekani kwa kipimo. Gharama hii ni mshahala wa takribani mwezi mzima katika maeneo mengine ya Afrika.

Gharama ya ARVs, ikiunganishwa na tuhuma pamoja na ukosefu wa habari zinawazuiwa maelfu wa wanawake wa Afrika kupata huduma muhimu za afya.

Zaidi ya hayo, umo ushahidi kwamba HIV unaweza uleta ukunzani dhidi ya Nevirapine. Wakati wanawake tayari wameambukizwa virusi vya HIV, juhudi za kupunguza usambazaji huwa kwa kawaida zinalengwa katika mbinu tulizo zijaja hapo mwanzo.

Walakini, hayo ni sehemu tu ya mikakati inayolenga kuzuia maradhi miongoni mwa wapenzi wanaotazamia kuwa wazazi na pia kuzuia ujauzito pasipo mpango kati ya wanawake wenye virusi vya HIV. Wakati ujauzoto umepangwa kuna njia mbadala ambazo zinaweza kupunguza hatari ya kuambukizwa.

Inakadiliwa kuwa katika dunia nzima 1% kati ya wanawake wote wajawazito wana virusi vya HIV. Katika hawa, karibu wote huishi katika nchi zinazoendelea kwenye upungufu wa huduma za afya.

Kwa hivi sasa, watoto 700,000 uambukizwa HIV kila mwaka, aidha wakiwa tumboni la uzazi, wakati wa kuzaliwa, au kupitia kunyonya. Kuna milioni tano ya watoto wenye HIV dunia nzima, 90% wakiwa wanaishi katika mataifa fukala. Ni rahisi kukandilia hali ya baadaye ya athari ya njia hii ya maambukizi. Watoto wazaliwapo na mama walio wagonjwa, kuna uwezekano wa kuwa mayatima wangali wachanga, na kukua katika umaskini, bila kupata masomo. Ni jambo la kawaida kwa mayatima kuishia barabarani za mji, au kugeukia uhuni na ukahaba wakitafuta kujikimu – Katika Africa Kusuni peke

yake, wamo watoto zaidi ya million moja katika hali hii. Ikiwa hawa watoto wenyewe wana HIV, tumaimi lao la kuishi ni ndogo mno. Tatizo hili ya kifedha na kiafya limekita mizizi.

Katika Afrika, mmoja kati ya wanawake watano chini ya miaka 25 wana HIV, kwa hivyo tatizo hili linaelekea kuwa njanga kuu. hali hii Ni ngumu kutatua, panapo hisia kali zinazo zingila swala la kunyonyesha na ukosefu wa habari yanafaya hali kuwa hoi. Mwelekeo mpya unalenga kutoa vipimo vya siri na mawaidha kwa wanawake wote waliokatika umri wa uzazi. Hili ni jaribio la kuvunja hali ya kutengwa na kukosa maarifa zinazozingila maradhi haya. Mataifa mengine ya Afrika kama vile Botswana na Lesotho, wanaanzisha vipimo vya lazima wakati wa ujauzito. Huu ndio mwelekeo uliopendekezwa na shirika la US Centre for Disease Control. Kama ilivyo katika mikakati yote ya kumasaidia wanawame wajawazito na watoto, ni muhimu kuelimisha na kuwezesha kinamama katika uaguzi na kutibiwa kwao.